

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



S. L.P 1055, ARUSHA
Simu : (027) 2503538/ 2507928
Nukushi: (027) 2505973
Barua pepe: rbcarusha@pccb.go.tz
Wavuti : www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

AGOSTI 04, 2020

**HATIMAYE TAKUKURU ARUSHA YAMKABIDHI ADVERA KYARUZI FEDHA
YAKE ALIYOKUWA AMEDHULUMIWA**

Ofisi ya TAKUKURU mkoa Arusha leo tarehe 04.08.2020 inamkabidhi mfanyabiasha ADVERA KYARUZI mkazi wa Mto wa Mbu wilayani Monduli, fedha kiasi cha Shilingi milioni tano, laki nne na elfu themanini (**Shilingi 5,480,000/-**). Kiasi hiki ni sehemu ya jumla ya shilingi milioni kumi na tano (Shilingi 15,000,000/-) alizokuwa amedhulumiwa na wafanyabiashara wenzake GERVAS ANDREA MOLLEL na JOSEPH CHRISTOPHER MOLLEL- wote wakazi wa Kata ya OLTRUMET wilayani Arumeru.

Fedha kiasi hicho cha Shilingi milioni kumi na tano (Shilingi 15,000,000/-) ni thamani ya mzigo wa mbegu za vitunguu wa Advera aliokuwa ameupakia kwenye FUSO yenye namba T 449 ATT lililokuwa linaendeshwa na JOSEPH CHRISTOPHER MOLLEL. Mzigo huo wa Advera na mizigo mingine kama hiyo ya watuhumiwa walikubaliana kwenda kuiuza Uganda, lakini kwasababu wanazozijua watuhumiwa, hawakupoleka mzigo huo na hawakutaka kumrejeshea Advera mzigo wake wala kumlipa fedha za mzigo huo. Tangu mwaka 2018, Advera amekuwa akifuatilia fedha zake kutoka kwa watuhumiwa bila mafanikio.

Baada ya ofisi ya TAKUKURU mkoa wa Arusha kupokea taarifa hizi kutoka kwa Advera, ilianzisha uchunguzi ambao umefanikisha ulipwaji wa kiasi cha fedha Shilingi milioni tano, laki nne na elfu themanini (**Shilingi 5,480,000/-**). Uchunguzi huu unaendelea ili kuhakikisha kwamba watuhumiwa wanalipa kiasi cha fedha kilichobakia.

TAKUKURU mkoa wa Arusha inawaasa wafanyabiasha na wananchi wa mkoa huu kwa ujumla kuendesha shughuli zao kwa uaminifu na kuacha kuwadhulumu wale wote wanaoshirikiana nao kwani watakapobainika kufanya hivyo, TAKUKURU haitasita kuwakamata na kuwachukulia hatua kali za kisheria.

Kupambana na Rushwa ni jukumu langu.

Imetolewa na:

Signed

James G. Ruge – 0738 150 063

KAIMU MKUU WA TAKUKURU (M) ARUSHA